

IYOYOO NALIA NAJILILIA MWENYEWE

Gosbert Damazo

Moderato

I
yo o na li a i
yo o na li a i

5

yo o na li a na i li li a du ni a i
yo o na li a na ji li li a mwe nye we

10

1. Mungu Ba ba tu na ku o mba u si ki li ze ki li o che tu u limwe ngu wa
Mungu Mwana tu na ku o mba njo o ha ra ka u tu o ko e u li mwe ngu wa
Mungu Ro ho M ta ka ti fu njo o ha ra ka tu ti e ngu vu u li mwengu wa

15

1. te ke te a vi u mbe wa ko wa a nga mi a
te ke te a vi u mbe wa ko wa a nga mi a
te ke te a vi u mbe wa ko wa a nga mi a.

2. Mwanadamu amegeuka amekuwa kama mnyama, mema yeye hayataki anataka yalo mabaya, Amri zako na za kanisa mwanadamu anazivunja, na za dola anazivunja amekuwa wake Rusifeli, Ni balaa limetusonga amani hakuna duniani, maadili yamemomonyoka shetani ametuelema.
3. Twavaa ngozi ya kondoo huku ndani sisi ni chui, tunatisha na hatukuifai Mungu Baba turekebishe, Kanisani tuko wa Mungu mitaani tu wa Ibilisi, tunatenda yasiyokufaa Mungu Baba tuhurumie, Binadamu kawa jeuri si mzee wala si kijana, haogopi na hatikisiki Mungu Baba tusaidie.
4. Umalaya umestawi uasherati nao uzinzi, ubakaji na ulawiti mwanadamu kafanya haki yake, Utoaji wa mimba changa na kuwatelekeza watoto, s-tarehe twazitafuta twausahau wajibu wetu, Wanaume na wanawake twaona wakana jinsi zao, Mungu Baba utuepushe hili balaa linatusonga.